**HALMASHURI YA WILAYA NACHINGWEA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA**

S.L.P 110NACHINGWEA
SIMU: 0652180502/0674441060/0653856486

December 2020

***KUMB.NA.A$_1$/NGSS/VOL.1/09***

MZAZI/MLEZI WA **……………………………………………………………………..….**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SEKONDARI YA WASICHANA NACHINGWEA KIDATO CHA KWANZA 2021**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa binti yako ………………………………………………………. Amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Nachingwea kwa mwaka wa masomo 2021.

Aidha Shule hii ya Sekondari ya Wasichana Nachingwea ni Shule ya kutwa inayo endeshwa katika mfumo wa Hostel hivyo gharama zote za chakula na huduma nyingine mzazi atahusika kwa asilimia mia moja. Mzazi/Mlezi unapaswa kukiri kwa maandishi kwamba utatoa ushirikiano wa kutosha bila usumbufu kwa uongozi wa shule.

Ni matumaini yetu kuwa wewe Mzazi/Mlezi utashirikiana na Uongozi wa shule katika malezi ili mwanao aweze kuitumia vema nafasi hii ya Elimu ya sekondari kwa manufaa yake na Taifa kwa ujumla.

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**(Jumatatu asubuhi) na mwanao anatakiwa afike shuleni bila kukosa ili taratibu za usajili zifanyike mapema na kuanza masomo rasmi mara moja.

Shule ipo karibu sana na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea Kata ya Boma umbali wa kilometa $2\frac{1}{2}$, upande wa kaskazini kutoka Stendi Kuu ya Mabasi.

Pamoja na barua hii naambatanisha na fomu ya Daktari kuhusu Afya ya mwanafunzi na fomu ya kukubali nafasi ili ujaze na kuja nazo shuleni tarehe tajwa (11/01/2021) isipokuwa fomu inayohusu sheria na kanuni za shule hii ni kwa ajili ya mwanafunzi mwenyewe awapo shuleni.

Karibu sana shule ya Wasichana Nachingwea

Nakutakia Maandalizi Mema.

**………………….**
Juma M Mchomvu
**K/MKUU WA SHULE**

**SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE KWA WANAFUNZI**

**UTANGULIZI:**

Sheria na taratibu hizi za shule zinalenga kat4ika kumpatia mwanafunzi malezi bora; yaani kumwandaa vema kitaaluma na kinidhamu, ili kumwezesha kuwa raia mwema, muungwana ma mstaarabu; aliye tayari kutumia uwezo wake wote kuitumikia jamii inayomzunguka na Taifa kwa ujumla.

**1. TAALUMA**

**Dira** ya shule ya Sekondari ya wasichana Nachingwea ni **"kutoa Elimu Bora na mazingira mazuri ya kujifunza"** na hatimaye kuwa shule bora ya kuigwa Tanzania.

Dhima ya shule ni **kuwa kituo cha ufahamu binafsi na kujitegemea** (Center of awareness and self reliance) ambapo itawasaidia kuwakomboa vijana **kiroho, kimwili na kiakili.**

Ili kufanikisha hayo (Dira na Dhima ya Shule) ni lazima;

(a) Kila mwanafunzi ahudhuriemasomo kwa muda wa siku zisizopungua mia moja na tisini na nne (194) kwa mwaka, ukiondoa siku za Jumamosi, Jumapili na sikukuu za Kitaifa

(b) Kama kutakuwa na sababu za msingi za mwanafunzi kutofika shuleni, ni jukumu la mzazi/mlezi kufika mwenyewe kutoa taarifa kwa mkuu wa shule au walau kutoa taarifa kwa maandishi kwa uongozi wa shule, mapema iwezekanavyo.

(c) Kila mwanafunzi anatakiwa kuingia darasani kwa wakatai na kukaa katika kiti chake kabla ya mwalimu wa somo kuingia na kuanza kufundisha.

(d) Mwalimu aingiapo darasani wanafunzi wote wasimame na kusalimia.

(e) Kila mwanafunzi audhurie vipindi vyote kwa mujibu wa ratiba ya siku.

(f) Kila mwanafunzi ni laziama afanye mazoezi na mitihani yote anayopewa na walimu wa masomo mbalimbali katika muda aliopewa. Na ni lazima kila mwanafunzi awe na daftari la mazoezi/majaribio kila somo.

(g) kila mwisho wa mwaka wa masomo, kila mwanafunzi atatakiwa kupata wastani usiopungua asilimia hamsini (50%). Adhabu kali atachukuliwa mwanafunzi atakayeshindwa kufika alama hizo. Kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza ni lazima angalau afikishe alama zisizopungua asilimia thelathini (30%), asipofikisha alama hizo atarudishwa shule za kata alikotoka.

(h) Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani. Atakayebainika kukiuka sheria hii, **atasimamishwa masomo na hatimaye kufukuzwa shule.**

(i) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa kimya muda wakati vipindi vinaendelea na wakati wa usiku ambapo wanafunzi wanapokuwa wanajisomea binafsi (Preparation Time).

(j) Ni lazima kila mwanafunzi atumie kiingereza kama lugha ya mawasiliano wakati wote anapokuwa shuleni. Hii itasaidia kuboresha taaluma kwa wanafunzi.

2. **TABIA NA MWENENDO (NIDHAMU)**

Shule ya sekondari ya wasichana Nachingwea inaamini kuwa tabia na mwenendo mzuri *(Nidhamu Bora)* ni ufunguo wa Taaluma Bora. Kwa hiyo inahimiza sana juu ya wanafunzi kuwa na tabia na mwenendo mzuri (Nidhamu bora). Hivyo;

(a) Kila mwanafunzi aheshimu Uongozi wa shule, ahaheshimu walimu, wafanyakazi wasio walimu, walezi wake na wanafunzi wenzake.

(b) Kila mwanafunzi aheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, Picha za Viongozi wa Taifa, Nembo na fedha za Taifa.

(c) Kila mwanafunzi ni lazima atumie lugha nzuri nay a heshima wakati wote akiwa shuleni na nje ya shule. Mwanafunzi **HARUHUSIWI** kutumia lugha ya matusi kati yake na mwanafunzi mwenzake na watu wote.

(d) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwasalimu wafanyakazi wote wa shule atakaokutana nao ndani na nje ya shule. Aidha, anatakiwa asimame na kuwasalimu mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita karibu yake.

(e) Ni lazima mwanafunzi awe mwadilifu, mwaminifu na mkweli wakati wote na ni lazima kuthamini na kuheshimu kazi za aina yote na kutunza heshima ya shule.

(f) Mwanafunzi hatakiwa kutoka darasani kwenda konana na mzazi/mlezi wake siku za kati ya juma, isipokuwa mzazi/mlezi ataonana na binti yako kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi tu. Na ukifika hapa shuleni ni lazima kuonana na walimu wa zamu au mwalimu mhusika kabla ya konana binti yako.

(g) Mwanafunzi haruhusiwi/ni marufuku kwa mwanafunzi kufanya mambo yafuatayo;

   (i) Kupiga kelele darasani au mabwenini wakati wa usiku na mara baada ya kutoka kujisomea (Preparation)
   (ii) Utoro wa kudumu au utoro wa rejareja (utoro wa vipindi), unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa.
   (iii) Kuonekana anapika au kuingia jiko la shule bila sababu maalum. Haruhusiwi kuingia jikoni kama si kiongozi.
   (iv) Kuonekana katika maeneo yafuatayo;Vilabu vya pombe (Baa), nyumba za kulala wageni (Guest House), bila sababu maaum, kumbi za starehe isipokuwa akiwa na wazazi/walezi
   (v) Kumiliki au kutumia simu shuleni.
   (vi) Kuendesha vyombo vya moto mabwenini au maeneno ya shule.
   (vii) Kuvuta sigara/bangi au kutumia madawa ya kulevya
   (viii) Kutoa chakula nje ya bwalo/ kulia chakula bwenini au darasani.
   (ix) Kunywa dawa ovyo, bila kupata ushauri wa wauguzi/daktari.
   (x) Kukaa/kuzagaa mbele ya jingo la utawala.
   (xi) Kuingia bila ruhusa chumba cha mwalimu, ofisi za walimu, maabara, jikoni na nyumba za wafanyakazi wasio walimu.
   (xii) Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali au ruhusa toka kwa uongozi wa shule.

## 3. AFYA NA USAFI

Afya na usafi ni sehemu muhimu ya Taaluma na nidhamu bora. Kama watu wanenavyo; Akili njema hupatikana katika mwili wenye afya, kwa hiyo, ni lazima;

(i) Kila mwanafunzi aonekane nadhifu.
(ii) Mwanafunzi ashiriki katika kusafisha mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na kufagia/kudeki vyumba vya madarasa, kuondoa buibui, kufuta vumbi kwenye vioo vya madirisha ofisini, madarasani na mabweni kila atakapotakiwa kufanya hivyo.
(iii) Kila mwanafunzi atunze vifaa vya kufanyia usafi atakavyokabidhiwa. Upotevu au uharibifu wa vifaa hivyo utagharimiwa na mwanafunzi ambaye atakuwa amehusika na uharibifu au upotevu wa vifaa hivyo.
(iv) Hauruhusiwi kuvaa nguo za nyumbani, khanga na mitindo isiyo ya heshima mfano; sketi fupi n.k
**(v)** Hauruhusiwi kujiremba, kama kupaka kucha rangi, kupaka midomo rangi, kupaka wanja, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kuvaa pete, hereni, bangili, mikufu, kuweka dawa kwenye nywele, kuwa na nywele ndefu, kucha ndefu n.k. Nywele zinatakiwa kuwa fupi zinazoshikika wakati wote. Mitindo yoyote ya nywele **HAIRUHUSIWI.**
(vi) Kuvuta sigara/bangi au kutumia madawa ya kulevya
(vii) Kuchelewa kufika/kuripoti shule na kutofanya usafi katika eneo alilopangiwa.

## 4. ADHABU

Mwanafunzi anaweza kusimamishwa na hatimaye kufukuzwa shule endapo atatenda moja au zaidi ya makosa yafuatayo;

(i) Wizi wa aina yoyote
(ii) Uasherati, na vitendo vyote vya kujamiana au kuleta hisia za kujamiana.
(iii) Uvutaji bangi, sigara au ulevi wa aina yoyote ( Pombe au madawa ya kulevya).
(iv) Kupiga au kupigana na mwanafunzi, wafanyakazi au watu wengine au kusababisha ugomvi.
(v) Makosa ya jinai.
(vi) Kuolewa
(vii) Kutoa mimba au kusababisha kutoa mimba.
(viii) Kugoma au kuchochea mgomo, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wote.
(ix) Kukataa adhabu iliyotolewa na uongozi wa shule au mwalimu kwa makusudi
(x) Kukutwa na simu ya mkononi shuleni.
(xi) Kuleta/kuletewa chakula shuleni toka nyumbani na kuja nacho mabwenini.
(xii) Utoro wa kudumu ( Zaidi ya siku 90)
(xiii) Kuhujumu au kuharibu mali za shule au mali za watu kwa makusudi.
(xiv) Kutumia lugha ya matusi kwa wanafunzi, wafanyakazi au watu wengine.
(xv) Kuandika kwenye kuta za shule; kuta za madarasa, ofisi, mabweni, maabara n.k.
(xvi) Kuasindwa kubadili mwenendo/tabia baada ya kuonywa mara nyingi.
(xvii) Kufanya udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani kama kuibia kwa mwanafunzi mwenzake, kuingia chumba cha mtihani na karatasi, nguo au vitambaa vilivyo na maandishi n.k.

**NB:** Kumbuka Shule ya Sekondari ya Wasichana Nachingwea ni shule maalumu, hivyo basi binti yako anatakiwa afaulu zaidi ya alama 30% mtihani wake wa mwisho wa mwaka wa masomo, chini ya alama hizo atatakiwa kurudishwa katika shule yake kataalikotokea.

## 5 MAHITATAJI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NACHINGWEA.

### A. SARE YA SHULE

Shule inasisitiza sana suala la umuhimu wa wanafunzi kuvaa sare za shule; zilizoshonwa vizuri na kukidhi matakwa na heshima stahiki. Ni lazima kila mwanafunzi avae sare ya shule wakati wote akiwa shuleni kama ifuatavyo;

(i) Sketi ndefu mbili za rangi ya ugoro (Brown)
(ii) Mashati mawili mapya meupe- tetroni mikono mifupi au Nusu kanzu na Juba kwa wanaovaa Hijab.
(iii) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba visivyokuwa na kisigino kirefu jozi mbili.
(iv) Soksi nyeupe jozi mbili kwa ajili ya sare
(v) Magauni mawili ya rangi ya zambarau kwa ajili ya kazi za nje yenye mikono mirefu na Juba lake kwa wanaovaa hijab au mikono mifupi kwa wasiovaa ( Shamba Dress)
(vi) T – Shirt 1 (Maelekezo atapewa Shuleni) na Sweta moja (Brown)

### B. SARE ZA MICHEZO

(i) Raba nyeupe kwa ajli ya michezo jozi moja
(ii) T – Shirt Bluu bahari 1.
(iii) Traki 1 nyeusi yenye michirizi meupe kushuka chini.

### C. MAHITAJI MENGINE

(i) Daftari 10 kubwa (Counter book QUIRE 3) na 10 za kawaida
(ii) Mathematical Set (Mkebe)
(iii) Mathematical Table ( Four Figure)
(iv) Godoro 1 jipya la sponji ( futi $2\frac{1}{2}$kwa futi 6)
(v) Sanduku lenye kufuli (TRANKA LA CHUMA)
(vi) Chandarua (Neti) 1
(vii) Foronya 2 na mto 1
(viii) Shuka mbili za rangi ya bluu bahari (Light blue)
(ix) Ndala za kuogea jozi 1
(x) Taulo moja
(xi) Ndoo ndogo mbili mpya na kopo la kuogea
(xii) Mswaki na dawa ya menoi
(xiii) Fagio ya chelewa yenye mpini mrefu/fagio ya kawaida
(xiv) Chanuo/kitana cha nywele
(xv) Aje na bakuli, sahani, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula
(xvi) Jembe jipya moja lenye mpini na panga kwa ajili ya usafi wa mazingira.

(xvii) Matibabu na mfuko wa afya ya jamii (CHF) 15,000/= (5000/= kwa ajili ya CHF na 10000/= kwa ajili Afya na matibabu. Kwa wenye Bima ya Afya, watachangia Tsh. 10,000/= tu.

(xviii) Mchango wa ununuzi wa solar SH. 8,000/=
Rim 1 ya kufanyia mazoezi na Mitihani ya ndani, Wilaya na Mkoa

.

**5. CHAKULA**

Mzazi/mlezi unatakiwa kugharamiachakula na mahitaji mengine kama ifuatavyo;

| **S/N** | **MAHITAJI** | **GHARAMA ZAKE** |
|---|---|---|
| 01 | CHAKULA | 438000 |
| 02 | WAPISHI | 20000 |
| 03 | MATIBABU NA CHF | 15000 |
| 04 | MATRON | 10000 |
| 05 | MAJI | 30000 |
| 06 | MLINZI | 10000 |
| 07 | NISHATI MBADALA[SOLAR] | 8000 |
| | **JUMLA KUU** | **531,000/=** |
| | | |

**NB;**Gharama hizi zitalipwa awamu nne kwa mchanganuo ufuatao;

- Awamu ya Kwanza,mwezi wa 1( JANUARI)= Tshs [231,000] laki mbili,thelathini na moja elfu .
- Awamu ya Pili mwezi wa 4 ( APRIL ) =Tshs [100,000] laki moja.
- Awamu ya Tatu mwezi wa 7 (JULAI)=Tshs [100,000] laki moja,
- Awamu ya Nne mwezi wa 9 (SEPTEMBA) =Tshs [100,000] laki moja.

.

**NB:Mzazi/Mlezi unashauriwa kuleta fedha kwa ajili ya mahitaji haya, kwani vyakula halisi vikiletwa kwa wingi vikachelewa kutumika vinaweza kuharibika na kusababisha hasara**.

**KATAZO:**

**Ni marufuku kwa mzazi/mlezi yeyote kumletea chakula chochote mwanafunzi akiwa shuleni. Akikutwa na chakula bwenini ni kosa la kufukuzwa shule papo hapo.**

Jumla ya gharama ya chakula, Matibabu na Afya na mahitaji mengine ni **Tshs531,000/=** kwa mwaka. Fedha zote zilipwe benki ya **NMB** tawi la Nachingwea akaunti namba **70410003958.** Jina la akaunti ni **Nachingwea Girls Reccurent A/C.** Aidha baada ya kulipia Benki unatakiwa kuleta hati ya malipo husika shuleni.Hatupokei fedha mkononi, fedha zote zilipwe benki kwenye akaunti iliyotajwa.

## 6. FEDHA ZA MATUMIZI

Mzazi/Mlezi unatakiwa umpatie binti yako fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi binafsi madogomadogo ya kila siku, mfano; mafuta ya kupakaa, dawa ya meno, sabuni n.k.

## 7. NGUO BINAFSI

Mzazi/mlezi, binti yako anatakiwa aje na magauni ya shule yaliyoagizwa hapo awali, nguo za ndani, kanga/kitenge doti moja na nguo za michezo tu. Tafadhali, asilete mavazi mengine zaidi ya hayo yaliyotajwa. Nguo za kawaida za nyumbani hazitakiwi awapo shuleni na awapo shuleni anatakiwa avae sare za shule tu.

## 8. DINI NA IBADA

Shule inatambua uhuru wa kuabudu kama ilivyoainishwa kwenye katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo kila mwanafunzi ataruhusiwa kuamini na kushiriki shughuli za dini yake au madhehebu yake ili mradi imani na shughuli hizo haziathiri sheria na taratibu nyingine za shule, hususani zinazohusu ustawi wa taaluma na nidhamu. Hivyo;

(i) Ni lazima kila mwanafunzi ahudhurie kipindi cha dini kama ilivyompasa kufanya katika vipindi vingine vyote vilivyoainishwa kwenye ratiba ya shule.

(ii) Shule haitaruhusu mwanafunzi yeyote kubadili dini yake akiwa shuleni bila ya ridhaa ya maandishi toka kwa mzazi/mlezi wake.

(iii) Wanafunzi wataruhusiwa kwenda kwenye nyumba za ibada kulingana na siku husika. Ijumaa kwa waislamu na Jumamosi na Jumapili kwa wakristo.

(iv) Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujihusisha na DINI ZISIZO RASMI kama DINI ZA ASILI, DINI ZA KUABUDU MASHETANI n.k.

## 9. LIKIZO

Kutokana na sheria iliyowekwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, mwanafunzi anatakiwa kwenda nyumbani kwa wazazi/walezi wake halali. Iwapo mwananfunzi atapenda kwenda kwa ndugu, marafiki ni lazima wazazi/walezi waandike barua kwa Mkuu wa shule ili kuthibitisha kwamba wametoa ruhusa.

Mzazi/Mlezi unatakiwa kumleta binti yako shuleni mwenyewe wakati wa kufungua shule na kumfata shuleni wakati wa kufunga shule. Mwanafunzi asiyefuatwa na mzazi/mlezi wake atabaki shuleni.

**JAMAA NA MARAFIKI**

Tafadhali, mzazi/mlezi andika hapa chini orodha ya ndugu, marafiki na jamaa ambao wanaweza kumtembelea binti yako akiwa shuleni;

| JINA | ANAPOISHI | UHUSIANO | SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**10. TARATIBU ZA KUKAMILISHA KABLA YA KUANZA MASOMO/SHULE**

Kabla ya kuanza masomo, mwanafunzi anatakiwa kukamilisha kujaza fomu zifuatazo;

(i) Fomu ya daktari kuhusu afya ya mwanafunzi

(ii) Fomu ya kukubali nafasi aliyopewa/aliyochaguliwa

(iii) Unatakiwa kuleta nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate ) ili kuthibitisha uraia halali wa mwanafunzi. Vyeti vinapatikana ofisi ya Mkuu wa Wilaya

FOMU No. 1

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**

NACHINGWEA GIRLSSECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 110
**NACHINGWEA.**
DATE………………………
***REF. No. ………………………………***

To: The medical officer,
………………………………………..
………………………………………..
………………………………………..
**REF**:………………………………………………………(Name in full please examines the above named student as to her physical and mental fitness for a full time student)
The examination should include the following category;

(a) Eyesight (b) Hearing (c) Speech (d) Limbs (e) Venereal diseases (f) Leprosy
(g) Epilepsy (h) Neurosis (i) Pregnancy (j) Other serious diseases e.g Asthma, TB, e.tc

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a Government Medical Officer).
I have examined the above named student and consider that she is fit/unfit for full time student.

(i) Eyesight
………………………………………………………………………………..…………………..
………..
(ii) Hearing
……………………………………………………………………………………………………….
…………..
(iii)Speech
………………………………………………………………………………………………………
……………
(iv)Limbs
………………………………………………………………………………………………………
…..…………
(v) Venereal diseases…………………………………………………………………………...
(vi)Leprosy
………………………………………………………………………………………………………
………..…..
(vii) Epilepsy
………………………………………………………………………………………………………
..…………

(viii) Neurosis
…………………………………………………………………………………………………….
.…………

(ix) Other serious diseases e.g Asthma ………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………….

(x) Tuberculosis
(TB)...……………………………………………………………………………………….
…....

(xi) Pregnancy
……………………………………………………………………………………………………
…………..

**Other comments**
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………..

**Name** ……………………………………………...……… **Date** ……………………..…**Signature** ……………………….

**STATION** …………………………………………………….. **DESIGNATION** ………………………………………………

NB: I requested this form to be returned to the school in sealed envelope

FOMU No. 2

## UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI WA KUKUBALI MAAGIZO YA SHULE

Mimi ……………………………………………………………………. (JINA LA MZAZI/MLEZI) mzazi/mlezi wa ………………………………………………………… nakubali kuzingatia maagizo yote yaliyotolewa katika fomu hii ya kujiunga na shule ya sekondari ya Wasichana Nachingwea kwamba kwa muda wote mwanangu atakapokuwa hapo nitahakikisha kwamba namhudumia kwa kumpatia mahitaji yote ya msingi ikiwemo kumlipia mchango wa chakula ulioainishwa katika fomu ya maelekezo kinyume na hapo nitakuwa sijatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi

Hivyo basi, endapo nitakiuka maagizo/maelekezo hayo nipo tayari kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kumhamisha mwanangu shule kwa kushindwa kumgharamia mchango wa chakula.

**Jina la mzazi/mlezi** …………………………………………….... **Tarehe**……………………………….

**Saini ya mzazi/mlez**i …………………………………………… **Tarehe** ………………………………